TANGAZO LA SERIKALI Na. 1042 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MABADILIKO YA MSITU ENEO LA WA HIFADHI WA TAIFA NJOGE YA MWAKA 2024

KWA KUWA, Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge ulitangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 393 la Mwaka 1954 kuwa Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge;

KWA KUWA, Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kufanya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge;

NA KWAKUWA, Waziri, kwa kuzingatia Sheria ya Misitu Sura ya, ambayo, pamoja na masharti mengine, inamtaka Waziri anapokusudia kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa, kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge.

Madhumuni ya

3. Madhumuni ya mabadiliko ya eneo la Msitu

tangazo

wa Hifadhi wa Taifa Njoge ni-

(a) kujumuisha eneo lote la ardhi ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa Njoge baada ya eneo hilo kupimwa upya kwa kutumia njia za upimaji na uchoraji ramani za kisasa; na

(b) kuhifadhi baioanuwai, vyanzo vya maji ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Njoge yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA YA KONGWA NA KITETO

MSITU WA HIFADHI WA NJOGE

Makadirio ya eneo: Hekta 1007.61 au Kilometa za Mraba 10.08 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Njoge linalopatikana Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 2855 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 1042 (Linaendelea)*




Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*